

Bwana ni mfalme

sikukuu ya kugeuka sura yake Bwana
Zaburi 96

Musique: Bernard Misangi

♩ = 80

Musical score for 'Bwana ni mfalme' in 4/4 time, key of D major. The score consists of two systems. The first system has four measures. The lyrics are: Bwa - na ni mfal me a li ye ju u ya du ni a yo te. The second system has one measure, starting with a measure rest of 5 measures.

1. Bwana ni mfalme; dunia ishangilie,
Visiwa vingi vipate furaha.
Mawingu ya giza yanamzunguka.
Hukumu na haki ni msinji wa kiti chake.
2. Umeme wake unaangaza ulimwengu;
Nchi ikaona, ikatetemeka
Kama nta, milima inayeyuka
Mbele ya Bwana wa dunia nzima.
3. Mbingu zinatangaza
Haki yake
Na mataifa yote
wameona utukufu wake.